# SPEAK@HOME

SHUGHULI ZA KUZUNGUMZA NA KUSIKILIZA | #9

Lexia ENGLISH LANGUAGE DEVELOPMENT

Kuzungumza na mtoto wako kwa lugha ya (za) nyumbani kwako na kushiriki tamaduni na uzoefu wako naye husaidia kuimarisha mafunzo yake ya Kiingereza. Tumia michezo na shughuli hizi za kufurahisha katika lugha yoyote ili kusaidia ukuaji wake wa jumla wa lugha.

## Studio ya Sanaa

1. Chukua karatasi na zana za kupaka rangi.
2. Chukua nafasi kuchora mandhari kutoka kwenye kitabu, filamu au kipindi cha runinga kipendwa cha mtoto wako.
3. Baada ya kila nafasi, ulizaneni kuhusu mandhari hayo. Tumia maswali yafuatayo ili kuongoza mazungumzo yako:
   - Ni kipi kinafanyika kwenye mandhari haya?
   - Fafanua ______.
   - Niambie kuhusu ______ yake.
   - Ni nini ilifanyika wakati ______?
   - Ni kwa nini mhusika huyu ______?
   - Ni kipi kilishangaza kuhusu ______?

**Mfano:**

*Kwa nini mhusika huyu hakwenda kwenye duka? Alikuwa anaenda dukani, lakini alienda mbugani badala yake.*

## Igiza

1. Chagua hali isiyo ya ukweli kutoka kwenye orodha hii:
   - kupatana na mgeni wa angani
   - maisha kama nguva
   - kugundua kuwa una nguvu isiyo ya kawaida
   - kushinda Kombe la Dunia
   - maisha kama mhusika wa kitabu wako kipendwa
   - kuendesha zimwi
2. Mwambie mchezaji mmoja aigize.
3. Wachezaji wengine wanapaswa kuchukua nafasi kukisia hali hiyo isiyo ya ukweli kwa kutumia sentensi kamili.

**Mfano:**

*Niambie kuhusu chombo cha anga.*
*Eleza umuhimu wa bimu ya leza.*
*Je, umekuwa ukigundua galaksi kwa muda gani?*
*Je, mgeni wa anga alienda kijijini?*

## Maabara ya Kusikiliza

Soma kwa sauti au hadithia. Unahitaji mawazo ya hadithi? Chagua moja ya hizi:

- tukio muhimu kwa maisha yako
- wakati kitu kisichotarajiwa kilifanyika
- changamoto uliyokumbana nayo
- uamuzi mkubwa ambao ulilazimika kufanya
- yule mtu wa kupendeza zaidi unajua
- ziara uliyoenda mahali pa kupendeza

Kisha uliza maswali kutoka kwenye orodha iliyo hapa chini:

- Fafanua ______.
- Eleza umuhimu wa ______.
- Kwa nini ______?
- Ni kipi kilinishangaza kuhusu ______?
- Ulifuatia kufanya nini? ______?

Mhimize mtoto wako ajibu kwa kutumia sentensi kamili.

**Mfano:**

*Ni kipi kilinishangaza kuhusu chuo cha elimu? Hata kama ilikuwa kazi nyingi zaidi, ilifurahisha sana.*

Lexia © 2024 Lexia, a Cambium Learning Group company.

# SPEAK@HOME

SHUGHULI ZA KUZUNGUMZA NA KUSIKILIZA | #9

## Ongea

Panga mlo na mtoto wako. Shirikiana ili kuchagua mapishi na kutengeneza orodha ya ununuzi ya viungo ambavyo utahitaji. Kisha, tayarisha mlo pamoja na mle na familia yako. Tumia maswali yaliyo hapa chini ili kuongoza mazungumzo yako:

- Niambie kuhusu chakula chako kipendwa.
- Ni ______ ngapi ziko ______?
- Tunahitaji chumvi kiwango gani?
- Ni nini tunaweza kutumia ili kuongeza ladha zaidi?

Mhimize mtoto wako ajibu kwa kutumia sentensi kamili.

**Mfano:**
*Je, tunahitaji unga kiwango gani? Tunahitaji vikombe viwili vya unga.*

## Maswali 21

Chagua mchezaji wa kuanzia. Mchezaji huyo anachagua kitu kwa siri. Wachezaji wengine wanachukua nafasi kuuliza maswali ili kupata dokezo moja kwa wakati kuhusu kitu hicho cha ajabu. Wachezaji wanaweza kuuliza jumla ya maswali 21 kabla wawe na kisio.

Hapa kuna baadhi ya maswali unaweza kutumia ili kukusanya dokezo:

- Kitu hicho ni kina uzito upi?
- Kitu hicho ni gumu au nyororo?
- Ni nini itafanyikia kitu hicho ikiwa ______?
- Ni nini tofauti kuhusu kitu hicho kikilinganishwa na ______?
- Kitu hicho ni cha rangi gani?

**Mfano:**
*Ni nini tofauti kuhusu kitu hicho kikilinganishwa na mti? Huku mti una majani, kitu hiki hakina.*

## Kibanda cha Picha

Piga picha za wanafamilia wakikamilisha shughuli za kila siku, kama vile kupika au kujitayarisha kwenda shuleni. Kisha, tumia picha hizo kuzungumza kuhusu kile kila mwanafamilia anafanya. Tumia maswali yafuatayo ili kuongoza mazungumzo yako:

- Ni kipi kinafanyika hapa?
- Ni kipi kingine unaweza niambia kuhusu ______?
- Unafikiria ______ anafanya nini?
- Eleza ni kwa nini unafikiria ______ ana ______?
- Kwa nini ______?

Mhimize mtoto wako ajibu kwa kutumia sentensi kamili.

**Mfano:** *Unafikiria dada yako anafanya nini? Dada yangu anavalia mavazi ya kulala, kwa hivyo anaweza kuwa anaenda kulala.*

## Tembea

Gundua bustani au mbuga ya eneo na mtoto wako. Zungumza kuhusu kile mnachoona kwenye mandhari. Tumia maswali yafuatayo yaliyo hapa chini ili kuongoza mazungumzo:

- Fafanua mimea.
- Ni nini imesababisha udongo umomonyoke katika eneo hili?
- Ni nini ilifanyika wakati tuliondoa majani?
- Eleza ni kwa nini unafikiria ndege alitengeneza kiota chake hapo.
- Ni kipi kinashangaza kuhusu mto?
- Ni chindi wanagapi wako mitini?

Mhimize ajibu kwa kutumia sentensi kamili.

**Mfano:**
*Ni nini itafanyikia njia kukinyesha? Kukinyesha, njia inakuwa na matope.*

Lexia ENGLISH LANGUAGE DEVELOPMENT

© 2024 Lexia, a Cambium Learning Group company.

LE-SAH9SWA-1124